

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA MARA

Anuani ya Simu: "REGCOM".

Simu Nambari 028/2622004/2622005

Fax 028-2622764/2622324

E-mail: ras.mara@tamisemi.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,

S. L. P. 299,

MUSOMA,

TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMA

Ziara Rasmi ya Waziri Mkuu Mkoani Mara

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, anatarajia kufanya ziara rasmi ya siku saba kuanzia tarehe 15 hadi 21, 2018 Mkoani Mara.

Mhe. Waziri Mkuu atawasili wilaya ya Musoma Tarehe 15.1.2018 na kupokelewa na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Viongozi mbali mbali wa Mkoa pamoja na Uongozi wa Chama Cha Mapinduzi.

Katika Wilaya ya Musoma Mhe. Waziri Mkuu atapokea maelezo ya mradi wa upanuzi wa Uwanja wa ndege wa Musoma, kutembelea ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mwalimu Nyerere, kukagua Shule ya Sekondari ya Ufundi ya

Musoma, Kiwanda cha Samaki cha Alpha na kuzungumza na Watumishi wa Umma pamoja na kuwa na mkutano wa hadhara katika viwanja vya Shule ya Msingi Mkendo.

Tarehe 16.1.2018, Mhe.Waziri Mkuu akiwa Wilaya ya Rorya atakagua Kituo cha Afya Kinesi, kutembelea Shule ya Sekondari Buturi, kukagua miradi ya maji Utegi, kuongea na watumishi wa Umma wa Halmashauri ya wilaya ya Rorya. Pia atatembelea Kituo cha Polisi cha wana maji- Sota na kuongea na wananchi – Bubombi.

Tarehe 17/1/2018 Mhe. Waziri Mkuu amepangiwa kwenda Wilaya ya Tarime ambapo ataweka Jiwe la Msingi katika kituo cha Afya Sirari, kutembelea Shule ya Wasichana ya Borega , Shamba la mfano la Kahawa na Bwawa la Maji ambacho ni chanzo cha maji katika Mji wa Tarime, kufanya mkutano wa hadhara katika uwanja wa SabaSaba pamoja na kukutana na watumishi wa umma.

Tarehe 18.1.2018 Mhe. Waziri Mkuu atakuwa na mkutano wa hadhara katika mji mdogo wa Nyamongo, kukagua daraja la Mto Mara Serengeti/Tarime na kuweka jiwe la msingi kabla ya kuelekea Wilaya ya Serengeti.

Katika Wilaya ya Serengeti Mhe.Waziri Mkuu atatembelea mradi wa Hospitali ya Wilaya ya Serengeti, mradi wa mfano wa mifugo wa magereza, kuzungumuza na watumishi wa Umma na kuwa na mkutano wa hadhara katika uwanja wa Mbuzi uliopo katika mji wa Mugumu.

Tarehe 19.1.2017 asubuhi akiwa Wilayani Serengeti Mhe Waziri Mkuu atatembelea shule ya sekondari Rubanda na kufungua rasmi shule hiyo kabla kuelekea wilayani Bunda.

Aidha Mhe. Waziri Mkuu akiwa katika Wilaya ya Bunda atatembelea Zahanati ya Hunyari, Shamba la umwagiliaji Nyatwali, kiwanda cha mafuta cha Villian, mradi wa maji cha Kaswaka, kuzungumza na watumishi wa umma kisha kumalizia na mkutano wa hadhara katika uwanja wa Stendi mpya. Aidha tarehe 20.1.2018 asubuhi, Mhe. Waziri Mkuu ataembelea shamba darasa la utafiti wa Pamba lililopo kijiji cha Kisangwa kabla kuelekea Wilaya ya Butiama

Akiwa Wilaya ya Butiama, Mhe. Waziri Mkuu atatembelea Shule ya Sekondari ya Kidato cha Juu cha Bumangi, Chuo Kikuu cha Mwl. J.K Nyerere, kukagua mradi wa Daraja la Kyarano, Shamba la mbegu bora ya mhogo Rwamkoma, kutoa heshima kwenye kaburi la Baba wa Taifa, kuzungumza na watumishi wa umma na mkutano wa hadhara katika uwanja wa Mwenge.

Tarehe 21.1.2018 Wilaya ya Musoma Mhe. Waziri Mkuu atakagua Mradi wa Maji Mugango-Kiabakari-Butiama na kukagua nyumba za watumishi, chumba cha upasuaji na kuzindua Jengo la Mama na Mtoto katika Kituo cha Afya Murangi. Baada ya Hapo Mh. Waziri Mkuu ataongea na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma.

Hii ni mara ya kwanza Mhe Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kuwa na ziara rasmi Mkoani Mara. Aidha Uongozi wa Mkoa wa Mara unawasisitiza Wananchi kiujumla kujitokeza kwa wingi kumpokea Mhe. Waziri Mkuu.

Asanteni sana.

